TAARIFA FUPI YA WILAYA YA MBARALI

1. UTANGULIZI.

Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Wilaya tisa na Halmashauri kumi zinazounda Mkoa wa Mbeya. Wilaya hii ilianzishwa mnamo tarehe 7 Julai, 2000 kwa mujibu wa vifungu vya 8 na 9 vya Sheria ya Serikali za mitaa ya mwaka 1982 na kupatiwa cheti kilichosainiwa tarehe 5 June, 2003.

1.1 MAHALI ILIPO NA MIPAKA YAKE.

Wilaya ya Mbarali ipo kati ya nyuzi 33.40 na 35.40 Longitudo kuelekea upande wa Mashariki, nyuzi 7.41 na 9.25 kusini ya Ikweta. Upande wa Kaskazini Mashariki, inapakana na Wilaya ya Iringa Vijijini, upande wa Mashariki inapakana na Wilaya ya Njombe, upande wa Kusini kabisa inapakana na wilaya ya Mbeya na Kaskazini inapakana na Wilaya ya Chunya.

1.2. ENEO NA MATUMIZI YA ARDHI.

Wilaya ina jumla ya eneo la Kilometa za mraba 16,000 na mgawanyo wa matumizi ya ardhi ni kama inavyoonyesha kwenye jedwali No. 1.

JEDWALI I:

NA	MATUMIZI YA ARDHI	KM ZA MRABA	HEKTA	ASILIMIA YA UWIANO
1	Ardhi kwa ajili ya kilimo	3,215	321,500	20.09
2	Eneo la wanyama pori	5,200	520,000	32.5
3	Hifadhi ya Misitu	172	17, 200	1.1
4	Eneo la makazi	6,078	607,800	38.0
5	Uwanda wa Tambarare, vilima, maeneo oevu na ufugaji	2,590	259,000	16.2
	JUMLA	**16,000**	**1,600,000**	**108**

1.3. SURA YA NCHI

Wilaya ya Mbarali ipo uwanda wa chini wa tambarare wenye nyasi na sehemu kubwa ya Wilaya imepitiwa na Bonde la Ufa na maeneo yenye miinuko kwa upande wa Magharibi, ikiwa na mito mitatu ya kudumu. Vile vile Wilaya ina chanzo kikuu cha maji ambacho ni Mto Ruaha Mkuu ambao baadaye huungana na mto Rufiji na kumwaga maji katika Bahari ya Hindi.

Wilaya imegawanyika katika kanda tatu za **KIIKOLOJIA** ambazo ni Uwanda wa Msangaji, Uwanda wa kati wa Usangu na Tambarare za Kusini mwa Usangu.

JEDWALI II:

NA	KANDA	MAHALI ILIPO	ALTITUDE (M)	UDONGO WA MVUA	SHUGHULI KUU ZA KIUCHUMI
1	Uwanda wa Msangaji (kanda ya Kaskazini)	Ruaha National Park	1200-1800	- Udongo wa mawe wenye rutuba ndogo - Mvua milimita 500-900 kwa Mwaka - Unyevunyevu miezi 3-5	Eneo lipo Hifadhi ya Taifa ya Ruaha (RUNAPA)
2	Uwanda wa kati wa tambarare ya Usangu (Ukanda mkuu wa ufugaji)	- Ruiwa - Ut/Usangu - Rujewa - Mapogoro - Sehemu ya kata ya Mawindi	1000-1400	Udongo mweusi na kichanga Mvua mm 450-650 kwa mwaka Unyevunyevu miezi 3-4	Kilimo cha mazao ya: - Mtama - Uwele - Ufugaji - Mahindi - Mpunga

NA	KANDA	MAHALI ILIPO	ALTITUDE (M)	UDONGO WA MVUA	SHUGHULI KUU ZA KIUCHUMI
3	Tambarare za Kusini Usangu (ukanda wa kusini – kanda ya kilimo)	- Ilongo - Rujewa - Chimala - Mapogoro - Igurusi - Ubaruku	750-1000	Mvua haba mm 360-750	Kilimo cha mazao ya: - Mahindi - Karanga - Pamba - Kilimo cha umwagiliaji Mpunga - Ufugaji

1.4. HALI YA HEWA NA UOTO

Wilaya ya Mbarali ipo katika latitude inayoanzia mita 1,000 – 1,800 juu ya usawa wa Bahari. Wastani wa joto ni kati ya nyuzi 25c na 30c. Wastani wa mvua hutofautiana kati ya milimita 300-940, hata hivyo kuna misimu miwili yaani msimu wa kiangazi ambao huanzia mwezi Mei – Novemba na msimu wa mvua ambao huanza Desemba – Aprili

Kwa ujumla Wilaya yote iko ndani ya uwanda wa Tambarare katika Bonde la Usangu ambalo lina uoto wa Asili aina ya Mipogoro.

Hali ya Mvua kwa Miaka Mitano iliyopita ni kama ifuatavyo:

NA	MWAKA	WASTANI WA MVUA (MM)
1	2005/2006	300.00
2	2006/2007	800.00
3	2007/2008	450.00
4	2008/2009	400.00
5	2009/2010	412.80
6	2010/2011	428.00
7	2011/2012	473.96
8	2012/2013	216.48
9	2013/2014	770

Hali hii ya upunguaji wa Mvua, inaathiri sana uzalishaji wa mazao ya kilimo hususani mpunga ambao ndio tegemeo kuu la mapato yetu ya ndani.

1.5. MUUNDO WA UTAWALA NA MAKABILA.

Muundo na utawala wa Wilaya ya Mbarali ni kama inavyoonyesha kwenye jedwali.

JEDWALI III

TARAFA	MAJIMBO YA UCHAGUZI	KATA	VIJIJI	VITO NGOJI	KAYA	WAH. MADIWANI		
						KUCHAGU LIWA	KUTEULI WA	JML
2	1	20	103	713	69,888			

1.6 MAKABILA

Makabila makuu yaliyopo Wilayani Mbarali ni Wasangu, Wahehe, Wakinga, Wabena na Wanyakyusa. Vile vile yapo makundi madogo ya makabila wakiwemo Wasukuma, Wanji, Wabarbeig na Wagogo.

Makundi mengi ya makabila haya ni wakulima na wafugaji ambao walihamia bonde la Usangu kutoka Mikoa ya Arusha, Mwanza, Shinyanga, Singida na Dodoma.

1.7. IDADI YA WATU

Kufuatia sensa ya kitaifa ya idadi ya watu ya mwaka 2012, Wilaya ya Mbarali sasa ina jumla ya watu 300,517 ambao kati yao 145,867ni wanaume na 154,650 ni wanawake ikiwa na ukuaji wa 2.8%.

1.8. IDADI YA WATUMISHI.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ina jumla ya watumishi 2,527. Mahitaji ni watumishi 2,971 hivyo kuna upungufu wa watumishi wapatao 1,012 kama jedwali linavyoonyesha hapa chini;

JEDWALI IV

Na	IDARA/KITENGO	IKAMA ILIYOIDHINI SHWA	WATUMISHI WALIOPO	UPU NGUFU	ZIADA
1	Utawala na Utumishi	144	130	14	-
2	Fedha na Biashara	22	19	3	-
3	Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji	6	5	1	-
4	Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika	134	83	51	-
5	Mifugo na Uvuvi	128	48	80	-
6	Elimu ya Msingi	1648	1193	455	-
7	Elimu ya Sekondari	495	434	61	-
8	Maji	13	7	6	-
9	Ujenzi	30	21	9	-
10	Afya	688	365	323	-
11	Ardhi na Maliasili	26	21	5	-
12	Maendeleo ya Jamii	27	23	4	-
	JUMLA	**2,971**	**2,527**	**1,012**	**-**

1.9: MWENENDO WA MAPATO NDANI YA HALMASHAURI

Halmashauri imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo na ustawi wa jamii kupitia Mapato yake ya Ndani yanayotokana na vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ushuru wa mazao, ushuru kutokana na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri. Mwenendo wa mapato ya ndani ya Halmashauri ni kama ifuatavyo:-

JEDWALI V

NA	MWAKA	MAKISIO	MAPATO	ASILIMIA (%)
1	2007/2008	319,882,060	487,449,295	152
2	2010/2011	478,894,538	666,742,372	139
3	2009/2010	721,124,000	639,527,000	88.7
4	2010/2011	728,757,700	621,890,570	85.3
5	2011/2012	773,027,000	934,388,639	121
6	2012/2013	1,348,748,000	915,496,546	67.9
7	2013/2014	1,602,798,000	1,396,807,050.55	87.1
8	2014/2015	2,672,063,706	1,921,741,556.72	72

2.0: SHUGHULI ZA KIUCHUMI.

Uchumi wa Wilaya ya Mbarali unategemea kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa mali vijijini hasa sekta ya Kilimo, wastani wa asilimia 83 ya wakazi Wilaya ya Mbarali hujishughulisha na kilimo, shughuli zingine za kiuchumi ni pamoja na ufugaji, uvuvi na biashara ndogondogo; kwa ujumla wake pato la mkazi wa Mbarali ni shilingi 376,500/= kwa mwaka.

2.1 KILIMO

Asilimia 83 ya wakazi wa Wilaya ya Mbarali hujishughulisha na kilimo na ufugaji. Mazao muhimu ya chakula ni pamoja na Mpunga, Mahindi, Viazi vitamu, Mihogo, Maharage na Mtama. Hata hivyo mpunga huzalishwa kama zao la chakula na biashara. Mazao ya biashara ni Alizeti, Karanga na Mazao ya bustani.

Kutokana na hali ya hewa isiyotabirika na kupungua kwa mvua, Halmashauri imekuwa inawekeza katika Kilimo cha umwagiliaji.

Mpaka sasa, Wilaya ya Mbarali ina jumla ya skimu za umwagiliaji 80 zenye jumla ya hekta 78,953. Kati ya hizo skimu 34 zimeboreshwa zenye jumla ya eneo linalofaa kulimwa hekta 41,724 lakini zinazolimwa ni 23,519. Aidha skimu 46 hazijaboreshwa zengye jumla ya eneo linalofaa kulimwa hekta 37,229 lakini zinazolimwa ni 20,989.

Juhudi zinaendelea za kuboresha miundombinu ya skimu za kilimo cha umwagiliaji, kuwajengea uwezo wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija zaidi, Ujenzi wa miundombinu ya masoko (maghala na viwanda vya usindikaji) na kuboresha barabara za vijijini zipitike kwa urahisi.

2.2. MALIASILI

Wilaya ina utajiri wa maliasili mbalimbali ikiwa ni pamoja na misitu, wanyamapori, madini, ufugaji nyuki, samaki na sehemu ya hifadhi ya Taifa Ruaha, vilevile pori la akiba la Usangu.

3.0 HUDUMA ZA KIJAMII NA FURSA ZILIZOPO

3.1 ELIMU

Wilaya ina shule/vyuo kama ifuatavyo:

JEDWALI VII

NA	AINA YA SHULE	SERIKALI	BINAFSI	TAASISI	JUMLA
1	Shule za awali	100	-	2	102
2	Shule za msingi	103	2	-	105
3	Shule za sekondari	16	1	6	23
4	Vituo vya EWW	5	-	-	5
5	Vituo vya MUKEJA	12	-	-	12

- Idadi ya wanafunzi wa shule za msingi 51,999
- Idadi ya wanafunzi wa shule za sekondari 9,580
- Idadi ya walimu shule za msingi 1,193
- Uwiano wa walimu na wanafunzi 1:44

Kwa Mwaka wa masomo 2013 kiwango cha ufaulu kwa Elimu ya Msingi ni 70.0%
Wanafunzi waliofaulu na kuchaguliwa kuingia Sekondari ni 4143.Wanafunzi hao wote walipata nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza.

Kiwango cha ufaulu Kwa Elimu ya Sekondari ni; Kidato cha pili 94.87% na Kidato cha nne 71.23% (83.23%).

Aidha kwa upande wa Walimu hali halisi iko kama ifuatavyo:

JEDWALI VII

Sekta	Idadi ya Walimu			Asilimia ya Upungufu
	Wanaohitajika	Waliopo	Upungufu	
Elimu ya Msingi	1299	1193	106	8
Elimu ya Sekondari	597	506	91	15

3.2 AFYA

Wilaya ina vituo vya kutolea huduma ya afya kama ifuatavyo:

JEDWALI VIII

NA	VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA	SERIKALI	BINAFSI	TAASISI	JUMLA
1	Hospitali	1	-	1	2
2	Kituo cha afya	5	-	1	6
3	Zahanati	34	2	4	40

Kwa upande wa Rasilimali watu katika Idara ya Afya, hali iko kama ifuatavyo:

Shule	Idadi ya Watumishi			Asilimia ya Upungufu
	Wanaohitajika	Waliopo	Upungufu	
Hospitali ya Wilaya	211	164	47	22.3
Afya Kinga	26	11	15	57.7
Vituo vya Afya 5	195	87	108	55.4
Zahanati 34	510	185	325	63.7
JUMLA	**942**	**447**	**495**	**52.5**

3.3 MAJI

Wilaya ya Mbarali ina mtiririko wa mito inayoanzia safu ya milima ya kipengele na uproot, vyanzo hivi vimekuwa mtego wa maji ya bomba kwa vijiji 76 kati ya 93 vya Wilaya nzima.

JEDWALI VI:

NA	VYANZO VYA MAJI	IDADI	IDADI YA VIJIJI VINAVYONUFAIKA NA HUDUMA	IDADI YA WATU WANAONUFAIKA NA HUDUMA
1	Miradi ya kutegwa (gravity scheme)	10	52	160,848
2	Visima virefu (Borehole)	36	15	36,104
3	Visima vifupi (Borehole)	47	10	13,533
	JUMLA	**93**	**77**	**210,485**

3.4 BARABARA

Wilaya ina mtandao wa barabara zilizoanzishwa zenye urefu wa km 1,308.2 ambazo kati ya hizo, barabara zenye urefu wa km 305.5 zinahudumiwa na meneja wa TANROADS na km 1002.7 zinahudumiwa na Halmashauri. Barabara zinazohudumiwa na Halmashauri zimegawanyika kama ifuatavyo;

JEDWALI VII

NA	AINA YA BARABARA	UREFU
1	Barabara ya changarawe	Km 216.15
2	Barabara ya changarawe/udongo	Km 786.55

Aidha kuna km 555.95 ambazo hazijaandikishwa na zinahudumiwa na Halmashauri, baada ya kupitishwa na Baraza la Madiwani mwaka 1998 ili kuweza kufikia maeneo ya uzalishaji na utawala, ili kuboresha ujenzi wa uchumi katika Wilaya. Kati ya km 555.95 km 86.7 ni za changarawe na km 469.25 ni za udongo.

3.5 VYAMA VYA USHIRIKA

Vyama vya ushirika ni vyombo muhimu katika kumkomboa mwananchi kutokana na umaskini. Hali ya vyama vya ushirika katika wilaya ya Mbarali ni kama ifuatavyo:

JEDWALI VIII

NA	AINA YA USHIRIKA	WANACHAMA				MTAJI Tshs.'000,000			MIKOPO Tshs.'000'000	
		IDADI	MOJA MOJA	VIKUNDI	JUMLA	HISA	AMANA	AKIBA	TOLEWA	REJESHA
1	Ushirika wa Akiba na Mikopo	24	7,191	209	7,400	1282.5	430.9	2028.8	23.404.7	14,347.3
2	Ushirika wa usafirishaji wa mazao ya kilimo	3	86	-	86	12.4	-	-	-	-
3	Ushirika wa kilimo na masoko	8	4,168	14	4,182	316.6	-	-	-	-
4	Ushirika wa wafugaji	1	18	-	18	0.64	-	-	-	-
5	Ushirika wa kilimo na umwagiliaji	9	2,808	8	2,816	12.3	-	-	-	-
6	Ushirika wa biashara ya samaki	4	170	0	170	13.85	-	-	-	-
7	Wabeba mifugo	1	19			1				

	JUMLA	**50**	**15397**	**2028**	**15705**	**2593**	**378**	**2581**	**15801**	**12318**

3.6. VIKUNDI VYA KIUCHUMI VYA WANAWAKE NA VIJANA

Katika kuhakikisha umaskini unapungua kwa jamii wa wilaya ya Mbarali huduma ya mikopo kwa vikundi vya kiuchumi vya wanawake na vijana imekuwa ikitolewa tangu mwaka 1998 hadi 2013 kama inavyoonyesha:-

JEDWALI IX:
MIKOPO YA WANAWAKE CHINI YA MFUKO WA WDF

MWAKA	VIKUNDI	MKOPO TOLEWA	RIBA (10%)	MKOPO + RIBA	MAREJESHO	BAKI	% YA MAREJESHO
Bakaa 2006	82	70,993,000	9,122,800	80,115,800	79,626,554	1,233,454	99.39
2007	17	18,000,000	1,800,000	19,800,000	19,590,000	210,000	98.93
2008	14	15,200,000	1,520,000	16,720,000	16,180,000	540,000	96.77
2009	4	4,000,000	400,000	4,400,000	4,400,000	0	100
2010	12	10,350,000	1,755,000	11,385,000	11,385,000	0	100
2013	3	6,000,000	600,000	6,600,000	4,600,000	2,000,000	69.69
JUMLA	**32**	**124,543,000**	**15,197,800**	**139,020,800**	**135,781,554**	**3.983,454**	**97.66**

JEDWALI X:
MIKOPO YA VIKUNDI VYA VIJANA KUTOKA SERIKALI KUU NA H/WILAYA

MWAKA	KIKUNDI	MKOPO TOLEWA	RIBA (15%)	MKOPO + RIBA	MAREJESHO	BAKI	%
2006	7	3,000,000	450,000	3,450,000	3,450,000	-	100
2007	18	6,900,000	1,035,000	7,935,000	7,497,000	438,000	94.48
2008	4	2,000,000	300,000	2,300,000	1,885,000	415,000	81.96
2009	2	10,000,000	500,000	10,500,000	10,475,500	24,500	9977
JUMLA	**25**	**21,900,000**	**2,285,000**	**24,185,000**	**23,307,500**	**24,500**	

4.0: MIFUGO NA HUDUMA (MIUNDO MBINU)

Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa wilaya zenye ufugaji mkubwa wa mifugo kwa njia ya kienyeji na kisasa.

JEDWALI XI:
MIFUGO

NA	MFUGO	AINA YA MIFUGO				JUMLA
		MAZIWA	NYAMA	MAYAI	KIENYEJI	
1	Ngo'mbe	2,524	-	-	168,580	171,104
2	Mbuzi	71	-	-	83,302	83,373
3	Kondoo	-	-	-	38,491	38,491
4	Punda	-	-	-	4,081	4,081
5	Mbwa	-	-	-	11,789	11,789
6	Nguruwe	-	-	-	11,889	11,889
7	Kuku	-	-	4,273	245,780	250,053
8	Bata	-	-	-	33,125	33,125
9	Bata Mzinga	-	-	-	53	53
10	Kanga	-	-	-	2,612	2,612
11	Paka	-	-	-	3,911	3,911
JUMLA		**2,595**	**-**	**4,273**	**603,613**	**610,481**

JEDWALI LA XII:
MIUNDO MBINU (HUDUMA)

NA	MIUNDO MBINU	ILIYOPO	INAYOFANYA KAZI	MIBOVU	MAELEZO
1	Majosho	32	26	6	6 yanahitaji ukarabati.

NA	MIUNDO MBINU	ILIYOPO	INAYOFANYA KAZI	MIBOVU	MAELEZO
2	Machinjio kubwa (Slaughter House)	9	9	-	6 Yanahitajika kujengwa
3	Machinjio ndogo (Makaro)	17	17	-	Yanafanya kazi
4	Malambo	5	3	2	2 yanahitaji ukarabati.
5	Mabanda ya ngozi	3	3	3	3 Yahahitaji ukarabati na 6 yanahitaji kujengwa
6	Minada	7	7	7	7 inatakiwa kuboreshwa
7	Vituo vya afya (VHC)	7	7	7	7 vinatakiwa kujengwa
8	Vituo vya kupakia/kushushia mifugo	2	1	1	6 vinatakiwa kujengwa na 1 kinahitaji ukarabati
9	Maduka ya pembejeo za mifugo	21	21	-	Yanafanya kazi
10	Mabirika ya kunyeshea Mifugo	8	6	2	2 yanahitaji ukarabati na 9 yanahitaji kujengwa

5.0: UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA MWAKA 2013/2014.

Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ilipokea jumla ya **Sh.8,348,327,271** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka Serikali Kuu na Wahisani mbalimbali. Vilevile Halmashauri ilikuwa na salio anzia la **Sh.334,495,245** na hivyo kufanya kuwa na jumla ya **Shs.8,348,327,271.** Kati ya fedha hizo **Sh.7,399,192,417** sawa na **88%** zilitumika na **Sh.949,134,854.29** sawa na **12%** zikiwa ni bakaa kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

Salio anzia (Sh)	Mapato (Sh)	Jumla ya Mapato (Sh)	Matumizi (Sh)	Bakaa (Sh)
334,495,245	8,013,832,026	8,348,327,271	7,399,192,417	949,134,854.29

Fedha hizo zimetumika katika utekelezaji wa miradi ya sekta mbalimbali. Mchanganuo ufuatao hapa chini unaonyesha mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 kulingana na taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kufikia tarehe 30 Juni, 2014.

6.0. HALI YA MAZINGIRA

6.1 MISITU

Eneo la Misitu ya asili na Nchi kavu lina ukubwa wa km za mraba 7604.6, eneo lenye misitu ya Hifadhi ni km za mraba 17.4 eneo lenye misitu iliyopendezwa kuwa hifadhi ni km za mraba 162. Wakati uwanda wa tambarare na ardhi oevu lina ukumbwa wa km za mraba 776.

6.2. UVUVI

Hali ya uvuvi Wilayani Mbarali hutegemea zaidi Mto Ruaha mkuu, Tindiga la Ihefu, Mito, na Mabwawa. Mpaka sasa kuna mabwawa 260 ambapo 231 yanamilikiwa na watu binafsi na moja ni la Halmashauri ya Wilaya.

6.3. WANYAMA PORI

Eneo la pori la akiba ni kilomita za mraba 5200, eneo la mapori ya wazi huchukua kilometa za mraba 11,852. Aidha kuna aina mbili za uwindaji ndani ya wilaya (uwindaji wa kitalii na uwindaji wa kienyeji).

6.4. MIJI NA MAKAZI

Wilaya ya Mbarali ina Mamlaka ya mji mmoja mdogo wa Rujewa ambao ndio makao makuu ya Wilaya na miji midogo sita (Madibira, Ubaruku, Chimala, Igurusi, Ut/Usangu na Ruiwa. Kati ya miji hiyo ni miji 4 iliyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi (Planning Proposals).

6.5 VYANZO VYA MAJI

Hali ya vyanzo vya maji katika Wilaya si nzuri kwani vyanzo vingi vimeathiriwa na ukataji wa miti ya asili, uchomaji wa moto na uchungaji wa mifugo kiholela na kulima kwenye vyanzo vya mito.

6.6. KILIMO

Maeneo mengi ya kilimo yako wazi kwa sababu ya ufyekaji wa miti na vichaka kwa ajili ya kilimo. Aidha mashamba yaliyoko mabondeni hujaa maji kutokana na mafuriko baada ya mito kujaa maji. Pia kupitia mradi wa kilimo cha kijani kibichi, miche ya miti rafiki na mazao ya kilimo inakuzwa kwenye vitalu na kusambazwa kwa wananchi katika vijiji 25 mwaka 2012/2013 jumla ya miche ya mipogoro na matunda ilikuzwa na kusambazwa.

6.7 MIFUGO

Wilaya ya Mbarali ina eneo la km za mraba 16,000 na kati ya hizo km za mraba 1,485 zinatumika kwa malisho ya mifugo.

7.0. VIKWAZO /VIZINGITI

7.1. UKIMWI

Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi imekuwa ni tatizo kubwa katika wilaya ya Mbarali kwani umekuwa ukiathiri makundi mbalimbali hasa vijana ambao ndiyo nguvu kazi kubwa katika uzalishaji na matokeo ya upimaji wa Virusi vya Ukimwi ni kama inavyoonyesha.

JEDWALI LA XIII:

MWAKA	WALIOPIMA	WALIOKUTWA NA MAAMBUKIZI	% YA MAMBUKIZI
2002	946	136	14.4
2003	673	96	14.3
2004	932	141	15.1
2005	1,358	598	44.0
2006	1,317	548	41.6
2007	16,504	5,109	30.9
2008	7,513	3,005	39.9
2009	8,624	3,127	36.2
2010	6,362	2,053	32,2
2011	8,897	512	5.8
2012	10,375	924	8.9
2013	13,312	1,472	11
2014	16,445	2,544	15

7.2. MAGONJWA MENGINE

Magonjwa 10 makuu yanayoongoza kwa vifo kwa mwaka 2014/2015 kama inavyoonyesha hapo chini:-

JEDWALI LA XIV:

NA	MAGONJWA	CHINI YA MIAKA 5		ZAIDI YA MIAKA 5	
		WAGO-NJWA	VIFO	WAGO-NJWA	VIFO
1	Vichomi	1,763	25	2,131	34
2	Magonjwa ya njia ya hewa	853	8	769	26
3	Kuhara	853	0	769	26
4	Malaria	676	26	1,167	32
5	Magonjwa ya watoto wachanga	192	10	0	0

NA	MAGONJWA	CHINI YA MIAKA 5		ZAIDI YA MIAKA 5	
		WAGO-NJWA	VIFO	WAGO-NJWA	VIFO
6	Ajali	103	25	818	5
7	Upungufu wa damu	89	18	316	0
8	Kuungua	67	5	47	0
9	Sumu	40	5	97	9
10	UKIMWI	20	3	382	20
	JUMLA	**4,656**	**125**	**6,496**	**152**

8.0: UIMARA

Halmashauri ina umri wa miaka kumi na moja (11) na ni mtoaji wa huduma zote kwa jamii yake. Uimara ufuatao umeifanya Halmashauri kuwa ni chombo kinachotegemewa kuwa mtoaji wa huduma zake:-

- Uwezo wa kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine
- Kuwepo na Tindiga la Ihefu
- Miundo mbinu ya kilimo na mifugo.
- Uwezo wa kupitisha/kutumia sheria ndogo ili kuhimiza utoaji wa huduma
- Uzoefu wa kutumia rasilimali zake vizuri
- Wataalamu wenye ujuzi na uzoefu.

9.0. CHANGAMOTO

Halmashauri inatambua kuwa na udhaifu ufuatao:-

- Uvamizi wa wafugaji wa mifugo yao katika bonde la Usangu hasa katika Tindiga la Ihefu, ambalo lina hifadhi mtiririko wa maji yanayotumika kutoa umeme katika bwawa la Mtera.
- Matukio ya uchomaji moto ovyo kwenye misitu na mapori ya hifadhi.
- Uhaba wa masoko ya uhakika ya mazao mbalimbali ya kilimo.
- Njia duni za mawasiliano hasa barabara hivyo kufanya baadhi ya maeneo kutofikika kipindi cha masika.
- Wingi wa Mifugo.
- Kuchelewa kutolewa fedha kutoka Hazina na Wadau wengine wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Adha baadhi ya miradi ya maendeleo kutoletwa fedha zake zilizotengwa kwenye bajeti.
- Uhaba wa nyumba za kuishi watumishi.
- Upungufu wa watumishi.
- Mapato kupotea kutokana na mianya iliyokuwepo katika mikataba iliyopita ya mikusanyo ya ushuru.
- Kupungua kwa mapato kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao ya kilimo kutokana na upungufu wa mvua.
- Migogoro ya ardhi.

10.0. MKAKATI INAYOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

MIKAKATI YA MUDA MFUPI:

- Kuhuisha ushuru wa huduma.
- Kuandaa makisio yatokanayo na uzalishaji mazao.
- Kutoa elimu kwa walipa kodi ili waweze kulipa ushuru/kodi.
- Kuchukua hatua za kisheria kwa wakiukaji.
- Kuboresha sheria ndogo za ukusanyaji ushuru.
- Kuimarisha kitengo cha ukusanyaji ushuru.
- Kuboresha mikataba ya ukusanyaji ushuru.
- Kutoa elimu ya sheria ya ardhi na utatuzi wa migogoro.

MIKAKATI YA MUDA MREFU:

- Kuboresha miundombinu ya masokoya mazao ya kilimo na mifugo.
- Ujenzi wa kituo cha maegesho ya magari makubwa.

- Uanzishaji wa kiwanda cha kusaga kokoto -2013/14
- Kuanzisha mradi wa ukodishaji wa mitambo ya ujenzi wa miundombinu-2013/14.
- Kuboresha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji -2007/2008.
- Mradi wa unenepeshaji mifugo -2014/15.
- Usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani.
- Kuimarisha mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani.
- Kuimarisha barabara za vijijini na za kwenda mashambani kupitia DADP, TASAF, Road Fund na wahisani mbali mbali.
- Kuboresha uzalishaji wa kilimo na ufugaji kwa kuwezesha wakulima kupitia vikundi kupata zana bora, mbegu bora, uhamilishaji (usambazaji wa madume bora), mashine za kupandia na kuvuna mpunga.
- Ujenzi wa nyumba za watumishi kadri fedha zinavyopatikana.